

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



TAARIFA KWA UMMA

13 Aprili 2018

KUSAJILI VIFAA TIBA VINAVYOTUMIKA KWENYE VITUO VYA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA

1. Hivi karibuni Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ikishirikiana na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala ilifanya operesheni maalum ya kubaini uwepo katika soko la Tanzania wa vifaa tiba vinavyotumika kwenye vituo vinavyotoa huduma ya tiba asili na tiba mbadala.
2. Katika operesheni hiyo vifaa vingi vilikamatwa na wahusika kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa *Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219* pamoja na *Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala ya mwaka 2002*.
3. TFDA inaendelea na utaratibu wa kuteketeza vifaa vilivyokamatwa.
4. Kwa tangazo hili, wale wote wanaojihusisha na biashara husika ikiwa ni pamoja na matumizi ya vifaa hivyo wanaelekezwa kuacha kupotosha umma na kujipatia kipato kwa njia isiyo na maadili ya afya na tiba.
5. Ikiwa wanaofanya biashara ya vifaa husika wanaamini vinafanya kazi wanaelekezwa kuleta maombi ya kuvisajili kwa kufuata Mwongozo wa Usajili wa Vifaa Tiba wa mwaka 2016 au Mwongozo wa Usajili wa Vitendanishi wa mwaka 2016 ambayo

inapatikana kwenye tovuti ya TFDA (www.tfda.go.tz) au ofisi za Makao Makuu na Kanda.

6. TFDA ikipokea maombi ya usajili itafanya tathmini ya ubora, usalama na ufanisi na ikiridhika itavisajili kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo tajwa.
7. Wananchi mnaelekezwa kutotumia vifaa vilivyoko kwenye vituo vya tiba asili na tiba mbadala kwa kuwa havijasajiliwa na TFDA. Endapo mtakuta vifaa hivyo vinatumika tafadhali toeni taarifa kwenye ofisi za TFDA zilizo karibu yenu ikiwa ni pamoja na kwenye ofisi za Halmashauri au Polisi ili hatua ziweze kuchukuliwa mara moja.

Imetolewa na:

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Chakula na Dawa,
Barabara ya Mandela,
Mabibo External,
S.L.P. 77150,
DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 450512/2450751/658 445222/777
700002**

Barua pepe: info@tfda.go.tz

Tofuti: www.tfda.go.tz